




Mwelekeo Mpya:

Kuendesha Mazungumzo ya Kijamii juu ya Jinsia na Urejeshaji Ardhi

Mwongozo wa mwezeshaji

Yaliyomo



Nukuu inayopendekezwa

Crossland, M., Adeyiga, GK, Paez Valencia, AM (2023). Mwelekeo mpya: Mwelekeo Mpya: Kuendesha mazungumzo ya kijamii juu ya jinsia na urejeshaji ardhi-mwongozo wa mwezeshaji. World Agroforestry, Nairobi; Muungano wa Biodiversity International na CIAT, Roma; Chuo Kikuu cha Bangor, Bangor.

Shukrani

Kazi hii ilifadhiliwa na UK Partnering for Accelerated Climate Transitions (UK PACT) chini ya mradi wa "Kukuza suluhu za asili kwa ajili ya urejeshaji wa ardhi huku kuimarisha kikundi kazi cha kitaifa cha ufuatiliaji nchini Kenya", uliofanywa kwa ushirikiano na Serikali ya Kaunti ya Makueni, na kujenga kutoka shughuli za mradi wa Urejeshaji wa Ardhi Kavu uliofadhiliwa na IFAD-EC "Urejeshaji ardhi iliyoharibiwa kwa usalama wa chakula na kupunguza umaskini katika Afrika Mashariki na Sahel: kuongeza kiwango cha mafanikio kwa katika urejeshaji wa ardhi " na mradi wa Kukijanisha Afrika uliofadhiliwa na Umoja wa Ulaya, "Kukabiliana na Uharibifu wa Ardhi katika Afrika kwa Kuongeza Kilimo cha Kukijanisha". Tungependa pia kutambua na kuwashukuru wanawake wengi, wanaume na wawakilishi wa jamii walioshiriki katika mradi huu kwa muda wao na maarifa.

Shughuli zilizoainishwa katikamwongozo huu huteka sana kutoka kwa zana na mbinu zilizopo, zikiwemo:

- Leder S, Das D, Reckers A, Karki E. 2016. Participatory gender training for community groups: a manual for critical discussions on gender norms, roles and relations. Colombo, Sri Lanka: International Water Management Institute; Rome, Italy: CGIAR Research Program on Water, Land and Ecosystems.
- Jost C, Ferdous N, Spicer TD. 2014. Gender and inclusion toolbox: participatory research in climate change and agriculture. Copenhagen, Denmark: CGIAR Research Program on Climate Change, Agriculture and Food Security; Atlanta GA, USA: CARE International; Nairobi, Kenya: World Agroforestry Centre (ICRAF).
- Reemer T, Makanza M. 2015. Gender action learning system: A practical guide for transforming gender and unequal power relations in value chains. The Hague, Netherlands: Oxfam Novib.
- Hillenbrand E, Karim N, Mohanraj P and Wu D. 2015. Measuring gender transformative change: A review of literature and promising practices. CARE USA. Working Paper.
- Carden F, Smutylo T and Earl S. 2001. Outcome mapping: Building learning and reflection into development programs. International Development Research Centre

Imetolewa na Kands Collective - hello@kandscollective.com
 Utafsiri kwa lugha ya Kiswahili: Caroline Njoki
 Picha ya jalada: Kelvin Trautman

Kwa habari zaidi, wasiliana na:

- Mary Crossland Crossland@CIFOR-ICRAF.org
- Ana Maria Paez Valencia A.Paez-valencia@cgiar.org
- Catherine Muthuri (Project contact) c.muthuri@cifor-icraf.org

Kuhusu mwongozo huu

Mipango ya urejeshaji ardhi inaweza kuwa na athari tofauti kwa wanaume na wanawake kutokana na tofauti katika majukumu yao, wajibu, na upatikanaji wa rasilimali. Kupuuza jinsia katika kubuni na kutekeleza shughuli za urejeshaji kunaweza kuzidisha tofauti zilizopo za kijinsia na kudhoofisha mafanikio ya juhudi za urejeshaji.

Majadiliano ya Jamii ni chombo cha nguvu cha kuwezesha majadiliano ya wazi na yenye kuhusu mitazamo ya kijinsia, majukumu, vikwazo na fursa na jinsi zinavyoathiri maisha ya watu na uwezo wa kujihusisha na kufaidika kutokana na urejeshaji wa ardhi.

Mwongozo huu unatoa mwongozo wa hatua kwa hatua unaoeleza shughuli kadhaa zinazoweza kutumika wakati wa mazungumzo ya jamii ya saa 3 hadi 4. Kwa kushiriki katika shughuli hizi, washiriki watapata fursa ya:

- Kujadili majukumu na kanuni za kijinsia katika jamii yao na jinsi yanavyoathiri ushiriki wao na mandhari au mazingira.
- Tafakari jinsi kanuni za kijinsia zinavyoweza kuleta vikwazo au fursa kwa shughuli za urejeshaji wa ardhi na jinsi ya kuchukua hatua kukabiliana nazo.
- Jifunze kuhusu umuhimu wa jinsia katika kukuza matokeo ya usawa kwa urejeshaji wa ardhi na jinsi ya kutambua na kushughulikia changamoto zinazohusiana na jinsia katika kubuni, kupanga na utekelezaji wa shughuli za urejeshaji.

Kwa kutumia mazungumzo ya jamii, washiriki wanaweza kufaidika kutoka kwa nafasi salama na ya kushirikisha kuzungumza kuhusu majukumu na mitazamo ya kijinsia, pamoja na fursa za kukuza maarifa na ujuzi mpya. Kupitia igizo dhima, tafakari, na majadiliano, wanaweza kutumia ujuzi wa kutatua matatizo na kujadiliana na kuendeleza mawazo yao kuhusu jinsi ya kukuza usawa wa kijinsia na kuimarisha shughuli za urejeshaji ardhi.

Kwa nini jinsia ni muhimu kwa urejeshaji wa ardhi?

Wanawake wa vijijini mara nyingi wanahusika sana katika usimamizi wa mashamba na shughuli za urejeshaji ardhi. Hata hivyo, mara nyingi hukosa uwezo wa kufanya maamuzi na rasilimali muhimu ili kutekeleza majukumu haya kwa ufanisi. Kwa kuwa mipango ya urejeshaji ardhi mara nyingi inahitaji kazi kubwa na inahitaji maarifa spesheli, wanaweza kuwaelemea zaidi wanawake na kupunguza muda uliopo kwa shughuli nyingine za kiuchumi na zisizo za kiuchumi.

Kwa kuongezea, faida za urejeshaji sio kila wakati zinasambazwa kwa usawa kati ya zile zinazochukua gharama zake. Kwa mfano, wanawake mara nyingi wananyimwa fursa ya kudai faida kama hizo kutokana na umiliki wa ardhi usio na uhakika na ushiriki usio sawa katika kufanya maamuzi na udhibiti wa rasilimali za kilimo na kaya.

Kwa kuendeleza mazungumzo ya wazi, shughuli katika mwongozo huu zinasisitiza umuhimu wa kutambua na kushughulikia masuala ya kijinsia ili kufikia matokeo yenye ufanisi na usawa ya urejeshaji wa ardhi. Kupitia kukuza tafakari muhimu na mazungumzo juu ya mitazamo na mazoea ya kijinsia, wanahimiza jamii kutafakari juu ya jukumu la jinsia katika maisha yao na kuzingatia njia za kufikia usawa zaidi wa kijinsia.

JINSI YA KUTUMIA MWONGOZO HUU

Aikoni zifuatazo zinatumika kukusaidia kuabiri shughuli zilizoordheshwa katika mwongozo huu:



Maarifa ya vitendo ya kutia akilini



Takriban urefu wa muda unaohitajika kutekeleza shughuli



Idadi kamili ya washiriki kwa kila kikundi



Lengo la shughuli



Kwa nini shughuli ni muhimu kwa jinsia na urejeshaji wa ardhi

Je, ninahitaji nini?

Kujiandaa kwa mazungumzo ya jamii

Imetoholewa kutoka Leder na wengine (2016)

Ili kufanya mazungumzo ya jamii yenye mafanikio, ni muhimu kuwa tayari kwa vifaa sahihi. Utahitaji:



Karatasi na kalamu za rangi



Madaftari (kitabu cha kuchorea) na kalamu kwa kila mshiriki



Kadi za nafasi ya jinsia (ona Kiambatisho 1, uk.17)



Kadi za igizo dhima katika hali (angalia Kiambatisho 2, uk.18)



Vifaa vya shughuli za igizo dhima (kwa mfano, mavazi ya wanaume na wanawake, vitu vya nyumbani)

Ili kuhimiza majadiliano na ushiriki mzuri, inashauriwa kuvifanya vikundi kuwa vidogo, ikipendelewa kuwa na washiriki wasiozidi 15. Pia ni muhimu kuwa na mchanganyiko wa wanaume na wanawake katika makundi ya umri tofauti kuhudhuria mazungumzo na, ikiwezekana, waalike wanandoa kuhudhuria. Hii ni kwa sababu shughuli nyingi huzingatia uhusiano ndani ya kaya (haswa, shughuli 5 na 6) na hufanywa vyema na wanandoa.

Hatimaye, ikiwa unafikiri wanawake wanaweza kusitasita kuzungumza katika makundi mchanganyiko, unaweza pia kufikiria kuwa na vikundi tofauti vya kuachana na jinsia moja. Katika kesi hii, inashauriwa pia kuleta vikundi pamoja mwishoni mwa shughuli ili kila moja iweze kushiriki uchunguzi, umaizi, na hitimisho na jinsia tofauti, na kuwezesha mazungumzo juu ya jinsi wanaweza kujenga juu ya kila mmoja.

Ili kufanikisha warsha, inashauriwa pia kuwa na wawezeshaji wawili au zaidi. Hata kama mtu mmoja tu ndiye anayesimamia kwa wakati mmoja, mwezeshaji mwingine anapaswa kuwa mwangalizi na kuandika vidokezo. Katika vikundi vilivyo na washiriki wa kike, ni muhimu pia kuwa na wawezeshaji wa kike.



Jinsi ya kuwa mwezeshaji mzuri

Mwezeshaji ana kazi kadhaa muhimu ili kuhakikisha warsha ya urahisi na ufanisi. Majukumu haya ni pamoja na (yaliyotoholewa kutoka Leder na wengine 2016):

- **Kuhimiza ushiriki:** Lenga kujenga mazingira salama ambapo washiriki wanajisikia huru kujadili mada tete au changamoto na kuhakikisha kuwa kila mtu anahisi kujumuishwa katika mazungumzo na anaelewa kikamilifu shughuli.
- **Ongoza mazungumzo:** Ingawa ni muhimu kuhimiza ushiriki, jaribu kuongoza mazungumzo mbali na mada hasi, kama vile kusisitiza dhana potofu za kijinsia au maoni ambayo yanaweza kuwakera wengine. Badala yake, mkazo unapaswa kuwa katika kuhimiza mazungumzo ya kujenga, jumuishi ambayo yanakuza ushiriki wa pamoja.
- **Shikilia/fuata ajenda:** Ni muhimu kuheshimu wakati wa washiriki na kuzingatia ajenda. Zingatia muda, na usiruhusu kikundi kutumia muda mrefu kwenye mada moja.
- **Shiriki katika shughuli na majadiliano:** Ingawa mwezeshaji hatakiwi kutawala mazungumzo, inaweza kusaidia mara kwa mara kushiriki mawazo na uchunguzi wako wakati wa majadiliano. Hilo linasaidia kuonyesha kuwa haufahamu kila kitu na pia uko hapo kujifunza kutokana na mijadala.
- **Kugawana majukumu:** Sio lazima kufanya kila kitu peke yako. Ruhusu mtu mwingine anakili vidokezo au uliza washiriki wakushikie viigizo unapozungumza. Hii inaweza kusaidia watu walio kimya kuzungumza na kuweka watu wanaozungumza kuwa na shughuli nyingi.

Kwa kufuata vidokezo hivi, utakuwa umejitayarisha vyema zaidi ili kuwezesha mazungumzo ya jamii inayoshirikisha na kufana.

Shughuli za mazungumzo ya jamii

UTANGULIZI

Kutambulisha mazungumzo ya jamii

Imetoholewa kutoka Leder na wengine (2016)



Lengo: Shughuli ya kwanza ni kuwakaribisha washiriki na kuwasilisha kwa ufupi ajenda ya warsha, nyakati, na madhumuni, na kujitambulisha wenyewe kwa kila mmoja.



Tia akilini: Ili kuweka warsha chini ya saa 4, haipendekezwi kukamilisha shughuli zote sita katika mwongozo huu katika warsha moja. Badala yake, chagua kati ya mifano miwili ya warsha kutoka Jedwali 1 au unda ajenda mpya isiyozidi shughuli nne.



Wasilisha ajenda

Anza kwa kuwasilisha ajenda. Hii itawasaidia washiriki kuelewa wanachoweza kutarajia kutoka kwenye warsha, mada watakazoshughulikia na aina za mazungumzo watakayokuwa nayo. Eleza kwamba warsha ina shughuli nne za vikundi na kwamba shughuli hizi zinalenga mahusiano ya kijinsia, kisha pitia shughuli kwa shughuli ya ajenda (tazama Jedwali 1 kwa mifano ya ajenda ya warsha).



Unda nafasi salama

Kujadili jinsia inaweza kuwa dhana mpya kwa washiriki wengi. Sisitiza kwamba majadiliano yanahitaji sauti na hadithi za washiriki, na mazungumzo yanaweza kuleta masuala nyeti na yenye utata. Wajulishe washiriki kwamba kutokubaliana ni sawa na kwamba shughuli zinakusudiwa kuwa za kufurahisha na nyepesi!



Pata kufahamu kila mmoja

Mwisho, tambulisha kila mshiriki na mwezeshaji. Hili linaweza kufanywa kwa ubunifu kwa kuwafanya washiriki wajitambulisha kwa mtu mwingine kwa dakika moja hadi mbili. Kisha, waambie wamtambulisha jirani yao kwa kundi lote. Unaweza pia kuuliza kila mtu ajiandikie lebo ya jina katika kipande cha mkanda wa barakoa au kibandiko.

Jedwali 1. Mifano miwili ya jinsi shughuli katika mwongozo huu zinavyoweza kuunganishwa ili kuunda warsha ya mazungumzo ya jamii ya saa 3 hadi 4. Sehemu iliyobaki ya mwongozo huu itatoa maelezo ya kila shughuli.

MFANO 1		MFANO 2	
MUDA	SHUGHULI	MUDA	SHUGHULI
10 dakika	Kutambulisha mazungumzo ya jinsia	10 dakika	Kutambulisha mazungumzo ya jinsia
20 dakika	Shughuli 1: Kuelewa jinsia na jinsi	20 dakika	Shughuli 1: Kuelewa jinsia na jinsi
40 dakika	Shughuli 2: Nafasi ya Jinsia	40 dakika	Shughuli 2: Igizo dhima la kujadiliana
40 dakika	Shughuli 3: Igizo dhima la kujadiliana	40 dakika	Shughuli 5: Safari ya maono
40 dakika	Shughuli 4: Kukuza alama za maendeleo	40 dakika	Shughuli 6: Mti wa Usawazisho wa Jinsia
15 dakika	Zaidi ya warsha	15 dakika	Zaidi ya warsha

SHUGHULI YA 1

Kuelewa jinsia na jinsi

Imetoholewa kutoka Leder na wengine (2016)

20
dakika

Lengo: Katika shughuli hii, washiriki watachunguza tofauti kati ya jinsia na jinsi na vipi jamii na utamaduni unavyounda majukumu ya kijinsia.



Kwa nini ni muhimu? Jinsia ina jukumu kubwa katika kuunda maisha ya watu, na ni muhimu kutambua kwamba jinsia ni tofauti na jinsi ambayo ni sifa ya kibayolojia. Shughuli hii huwasaidia washiriki kuelewa jinsi jamii hujenga majukumu na matarajio ya kijinsia na "kwamba kuna tofauti kati ya kile tunachozaliwa na kile ambacho jamii inatambua kuwa" (Leder na wengine 2016).



Tia akilini: Kulingana na miktadha ya kitamaduni ya mahali hapo, unaweza kutaka kuzingatia urekebishaji wa shughuli ili kuwakilisha asili isiyo ya pande mbili ya jinsia. Chombo muhimu cha kuelezea utata wa jinsia ni dhana ya 'genderbread person' ambayo inashughulikia anatomia ya jinsi, utambulisho wa jinsia, kujieleza na mvutio wa jinsia: <https://www.genderbread.org>

HATUA YA
1

Kwanza, elezea kikundi kuwa shughuli hii inalenga kuelewa tofauti kati ya jinsi na jinsia.

HATUA YA
2

Uliza washiriki kufikiria maneno ya kwanza yanayokuja akilini wanaposikia maneno 'mwanamume' na 'mwanamke.' Andika majibu yao katika nguzo mbili kwenye karatasi : 'MWANAUME' na 'MWANAMKE'. Hakikisha umejumuisha baadhi ya maneno yanayoelezea sifa za kibayolojia kama vile 'uume' kwa mwanamume na 'matiti' kwa mwanamke.

HATUA YA
3

Mara baada ya orodha kukamilika, uliza washiriki maswali yafuatayo:

- Je, kuna neno lolote la 'mwanamume' linaloweza pia kuwaelezea wanawake? (Tia mviringo maneno haya kwa kutumia kalamu ya rangi, mfano samawati)
- Je, kuna neno lolote la 'mwanamke' linaloweza pia kuwaelezea wanaume? (Tia mviringo maneno haya kwa kutumia kalamu ya rangi, kwa mfano samawati)
- Ni mambo gani ambayo wanawake au wanaume pekee wanaweza kufanya? (Tia mviringo maneno haya kwa kalamu ya rangi tofauti, mfano kijani kibichi)

HATUA YA
4

Kisha eleza tofauti kati ya jinsi na jinsia ukitumia ufafanuzi ulio hapa chini:

- Jinsi ni sifa za kibayolojia na kisaikolojia za wanaume na wanawake wakati wa kuzaliwa. Kwa mfano, mifumo ya uzazi, sehemu za siri, kromosomu, na homoni).
- Jinsia ni muundo wa kijamii unaorejelea majukumu, tabia, na matarajio ambayo jamii huhusisha na kuwa mwanamume au mwanamke.

HATUA YA
5

Kisha, soma orodha ya sifa na tabia (tazama hapa chini kwa baadhi ya mifano) kwa mpangilio wa nasibu na uliza washiriki kukisia kama zimeamuliwa na jinsi au jinsia ya mtu. Hii inasaidia kuthibitisha kwamba kila mtu amelewa tofauti kati ya jinsi na jinsia.

JINSI	JINSIA
Hedhi	Kuvaa nguo
Kuwa mjamzito	Kuendesha tinga tinga
Kuzaa au kujifungua	Utunzaji wa watoto na wazee
Kunyonyesha watoto	Kupalilia
Kutoa mbegu za kiume	Kupika

HATUA YA
6

Sisitiza kwamba majukumu na wajibu ya kijinsia yanaweza kubadilika kwa wakati. Uliza washiriki wafikirie juu ya siku za nyuma na nini KIMEBADILIKA katika jamii yao kuhusiana na wajibu wa wakulima wa kiume na wa kike. Toa baadhi ya mifano, kama vile kuendesha baiskeli na pikipiki, kulima kwa ng'ombe, kuzungumza katika kikundi, au kuwajibika kwa pesa.

SHUGHULI YA 2 Nafasi ya Jinsia

Imetoholewa kutoka Leder na wengine (2016)

40
dakika

5-6



Lengo: Shughuli hii inalenga kuwasaidia washiriki kutafakari juu ya aina ya maamuzi na kazi inayofanywa na wanawake na wanaume katika urejeshaji wa ardhi, kilimo na shughuli za kaya na kuwahimiza kufikiria jinsi shughuli hizi zinavyoweza kugawanywa na mzigo wa kazi kusawazishwa.



Kwa nini ni muhimu? Inasaidia washiriki kuona kwamba mgao wa kazi na shughuli za urejeshaji mara nyingi husababisha mzigo mkubwa wa kazi kwa wanawake na jinsi kubadilisha jinsia inayowajibika kwa kazi maalum kunaweza kufanya kazi kuwa sawa zaidi kwa kila mtu.



Tia akilini: Utahitaji seti tatu za kadi za nafasi za kijinsia (moja kwa kila kikundi). Kadi hizi zijumuishe picha za shughuli mbalimbali za urejeshaji ardhi (kwa mfano, upandaji miti), shughuli za kazi za shambani na nyumbani, picha zinazwakilisha maamuzi mbalimbali ya shughuli za urejeshaji ardhi, na picha za mwanamume na mwanamke wakiwa wamesimama katika nafasi tofauti karibu na kila mmoja wao (angalia Kiambatisho. 1, ukurasa wa 17).

Ingawa tumetumia upandaji miti kama mfano, shughuli hii inaweza kutoholewa kwa mazoea tofauti ya urejeshaji ardhi, na sio upandaji miti pekee. Fikiria juu ya kazi tofauti na maamuzi yanayohusiana na mazoezi fulani ya urejeshaji na kuchukua na kuchapisha picha za kila shughuli. Mbadala, kama huna uwezo wa kufikia kamera/kichapishaji, unaweza kuchora shughuli kwenye kadi.

HATUA YA
1



Anza shughuli kwa kuweka picha za mwanamume na mwanamke wakiwa wamesimama katika nafasi tofauti karibu na kila mmoja kwa safu ili kuonyesha kuenea kwa leba kwa wanaume au wanawake. Eleza safu za picha, ukisema ikiwa inawakilisha kazi ya wanaume pekee, hasa kazi ya kiume, kazi inayoshirikisha jinsia zote mbili, hasa kazi ya wanawake, na kazi ya wanawake pekee.

HATUA YA
2

Weka kadi za picha za shughuli mbalimbali za upandaji miti katikati ya kikundi. Uliza kila mshiriki kuchukua picha ya shughuli ya upandaji miti.

HATUA YA
3

Uliza kila mshiriki aonyeshe picha yake kwa kikundi na kuelezea shughuli kwenye kadi yao. Kisha, uliza washiriki wajiadiliane na kuweka picha chini ya picha ya mwanamume na mwanamke wanayofikiri inawahusu (yaani, kazi ya kiume, hasa ya kiume, kazi inayoshirikisha jinsia zote mbili, hasa kazi ya wanawake, au kazi ya kike).



SHUGHULI YA 2 kuendelea

HATUA YA

4

Rudia hatua ya 3 na 4 kwa kadi za uamuzi wa mti (ukiziweka juu ya picha za mwanamume na mwanamke - kulingana na nani anahusika katika uamuzi), kadi za kazi ya shambani na kadi za kazi ya nyumbani (kuziweka hapa chini), mapka kadi zote kuwekwa.

HATUA YA

5

Uliza washiriki, “Je, hii inaonekana kama mzigo wa kazi sawa kwa wanaume na wanawake? Vipi kuhusu maamuzi ya upandaji miti?” Maswali ya ufuatiliaji, kama vile “Hii inaweza kusababisha matatizo gani kwa shughuli za upandaji miti?” na “Je, shughuli hii inaweza kufanywa na wanaume au wanawake pekee? Kwa nini?” inaweza kusaidia.

HATUA YA

6

Uliza, “Je, ungependa kubadilisha vipi nani anayefanya kazi gani na maamuzi katika siku zijazo, labda katika miaka mitano? Tafadhali panga upya kama ungependa kusawazisha kazi na maamuzi kwa njia tofauti.” Hatua hii inawahimiza washiriki kufikiria jinsi kubadilisha jinsia inayohusika na kazi fulani na maamuzi yanaweza kusaidia kufanya kazi kuwa sawa kwa kila mtu.



Tia akilini: Himiza washiriki kufikiria zaidi ya “siku zote imekuwa hivi.” Inaweza pia kusaidia kuwakumbusha jinsi mgao wa kazi tayari umebadilika kwa muda. Hii inaweza kuwasaidia washiriki kutambua kwamba mambo pia yanaweza kubadilika katika siku zijazo.



Photo: ICRAF/Ann Wavinya

SHUGHULI YA 3 Igizo dhima la kujadiliana

Imetoholewa kutoka Leder na wengine (2016)

40
dakika



5-6



Lengo: Lengo la zoezi hili ni kukuza uwezo wa kuhisi maono ya wengine kwa kuwafanya washiriki kuchukua nafasi ya jinsia tofauti na washiriki katika mazungumzo na washiriki wengine katika mazingira ya kilimo au kaya.



Kwa nini ni muhimu? Kwa kubadili majukumu ya kijinsia, washiriki wanapata kuelewa zaidi changamoto zinazokabili jinsia nyingine, na kusababisha kuongezeka kwa uelewa na kuthamini tofauti za kijinsia.



Tia akilini: Utahitaji seti ya kadi za igizo dhima ya hali (Kiambatisho 2, ukurasa wa 18), mavaazi ya kiume na kike kama vile skafu na mashati, na vifaa vya kilimo/kaya kama chungu cha maji, jembe, vikombe, n.k. Ikipendelewa, kila kikundi kuwa na washiriki wasiozidi 5-6. Ikiwa vikundi ni vidogo, majukumu ambayo hayajatumika yanaweza kutupiliwa mbali, na kama vikundi ni vikubwa, majukumu ya ziada ya “wanajamii” yanaweza kuongezwa (kwa mfano, uliza kundi kuunda wahusika wapya kwa igizo dhima lao). Kumbuka kwamba hili linapaswa kuwa zoezi la kufurahisha na nyepesi!

HATUA YA
1

Eleza washiriki kuwa watashiriki katika igizo dhima ambapo watakuwa wakivalia mavazi na kutenda kama jinsia tofauti. Sisitiza kwamba zoezi hili linakusudiwa kufurahisha na litawaruhusu washiriki kupata uzoefu wa jinsi mazungumzo yanavyotokea kutoka kwa mtazamo wa jinsia nyingine.

HATUA YA
2

Sambaza kadi za igizo dhima ya hali kwa kila meza na zisome kwa washiriki ikibidi.



Tia akilini: Kadi hizi za hali na maigizo dhima zinaweza kutoholewa kwa miktadha tofauti ya eneo na kitamaduni.

HATUA YA
3

Patia vikundi dakika 15 kuandaa igizo dhima fupi (dakika 3-5) kulingana na kadi ya hali waliyopokea. Kila mwanakikundi apewe kadi ya jukumu. Himiza vikundi kuwa bunifu katika maonyesho yao - kadiri igizo linavyofurahisha zaidi, ndivyo bora zaidi!

HATUA YA
4

Uliza kila kikundi kuigiza mchezo wao kwa vikundi vingine.

HATUA YA
5

Baada ya kila onyesho, uliza washiriki jinsi walivyohisi kuhusu kuchukua jukumu la jinsia nyingine. Uliza waliokuwa kati ya watazamaji walichofikiria kuhusu igizo na uhimize majadiliano juu ya majukumu ya kijinsia yasiyo ya kawaida na walichojifunza kutokana na zoezi hilo.



Photo: ICRAF/Alex Maina



Photo: ICRAF/Ann Wavinya

SHUGHULI YA 4 Kukuza Alama za Maendeleo

Imetoholewa kutoka kwa Mohanraj na Hillenbrand (2015)

40
dakika



Lengo: Lengo la zoezi hili ni kutambua masuala ya kipaumbele ya kijinsia na kuendeleza malengo ya pamoja, kwa lengo la kuwashawishi washiriki kuwa mabadiliko ya kijamii yanawezekana ndani ya muda mfupi.

HATUA YA
1

Gawa washiriki katika vikundi tofauti vya wanaume na wanawake. Waulize kufikiria kuhusu mabadiliko ambayo wangependa kuona kutoka kwa jinsia tofauti na waorodheshe kwenye karatasi ya chati mgeuzo. Unaweza kuchagua maeneo kadhaa ya mabadiliko kwa washiriki kuzingatia kulingana na majadiliano ya awali (kwa mfano, wakati wa shughuli ya nafasi ya jinsia) au katika muktadha wa mradi wako wa urejeshaji. Mfano wa makundi na mabadiliko yanaweza kujumuisha:

- Mgao wa kazi kijinsia na kugawana mzigo wa kazi kwa mfano, usimamizi wa pamoja wa miche ya miti (kumwagilia, kupalilia n.k).
- Majadiliano ya kaya, mawasiliano, na kufanya maamuzi (kwa mfano, maamuzi ya pamoja juu ya aina gani ya miti ya kupanda shambani).
- Udhhibiti wa mapato na mali za uzalishaji (kwa mfano, usajili wa pamoja wa ardhi na udhibiti wa mazao ya miti).
- Kujiamini na maelewano katika mahusiano (kwa mfano, uhuru wa kuhudhuria mafunzo juu ya mazoea ya urejeshaji ardhi).

HATUA YA
2

Mara baada ya kikundi kuorodhesha mabadiliko ambayo wangependa kuona katika kila kundi, waulize wapange mabadiliko muhimu zaidi ya 5-10 kulingana na yale wanayofikiri yatakuwa na athari kubwa kwa ustawi wa familia zao. Kisha, waulize watathmini ni mabadiliko gani kati ya hayo yanaonekana kuwa rahisi kufikiwa na yanaweza kutokea hivi karibuni, na ni mabadiliko gani yatahitaji uwekezaji na juhudi za muda mrefu zaidi. Hatua hii ni muhimu kwa sababu inasaidia watu 1) kutanguliza mabadiliko ambayo ni muhimu zaidi na 2) kufikiria kuhusu mabadiliko gani yanawezekana.



HATUA YA
3

Leta pamoja vikundi vya wanaume na wanawake na kuwasilisha viashiria vya kila kikundi. Jadili mifanano na tofauti kati ya alama za wanaume na wanawake.

- Uliza wanaume jinsi wanavyohisi kuhusu viashiria vya wanawake.
- Uliza wanawake jinsi wanavyohisi kuhusu viashiria vya wanaume.

HATUA YA
4

Uliza washiriki wafikirie jinsi wanavyoweza kufikia viashiria vyao vya kipaumbele vya mabadiliko na kunakili hatua muhimu zilizopendekezwa, na uwekezaji na usaidizi ambao ungehitajika ili kufikia mabadiliko rahisi na magumu.

SHUGHULI YA 5 Safari ya maono

Imetoholewa kutoka kwa Reemer na Makanza (2015)

40
dakika

1-2



Lengo: Zoezi hili linalenga kuwaongoza washiriki katika kufikiria shamba lao bora la siku zijazo na kuunda lengo linaloweza kufikiwa la urejeshaji.



Kwa nini ni muhimu?

Inasaidia washiriki kujifunza kanuni na hatua za kupanga, na inapofanywa kama wanandoa, kuunda malengo ya pamoja.



Tia akilini: Zoezi hili linapaswa kufanywa kibinafsi au na wanandoa kwa mwongozo kutoka kwa mwezeshaji. Watu/wanandoa huchora kila mmoja, lakini ni vyema wakae katika vikundi visivyo rasmi. Mwezeshaji anapitia polepole hatua akichora kwenye chati tupu kama mfano, huku kila mtu akichora kwenye madaftari/karatasi zao.

Ingawa shughuli hii inaweza kufanywa kama shughuli huru, inafanya kazi vizuri inapofanywa kabla ya Shughuli ya 6 - Mti wa Usawazisho wa Jinsia.

HATUA YA
1

Uliza washiriki kufikiria shamba lao katika siku zijazo. Je, wanatumia mazoea gani ya urejeshaji? Je, wanaweza kusikia na kuona nini? Nini hukua hapo? Aina gani za miti?

HATUA YA
2

Kwenye kipande cha karatasi ya chati, uliza washiriki wachore duara kubwa na, ndani yake, wachore picha za shamba wanaloliona - hili litakuwa chanzo cha maono yao kwa siku zijazo.



Photo: ICRAF/Ann Wavinya

HATUA YA
3

Mara baada ya kila mmoja kuwa na maono yake ya siku zijazo kukamilika, uliza washiriki kutoa maono yao na kubainisha mada zozote zinazofanana (kwa mfano, mabwawa ya shamba, miti ya miembe, kutengeneza ua n.k.). Uliza mwanakikundi mmoja atoe taarifa kwa kikundi kikubwa kuhusu vipengele vya kawaida vya maono ya kikundi chao.

HATUA YA
4

Kurudi kufanya kazi binafsi au kama wanandoa, uliza washiriki kuchagua shughuli moja ya urejeshaji ardhi kutoka kwa maono yao ambayo ni muhimu kwao na ambayo inaweza kufikiwa au kuleta maendeleo makubwa na yanayoonekana katika takriban miezi 18.

HATUA YA
5

Kisha, uliza washiriki wachore duara kubwa kwenye kona ya juu kulia ya ukurasa inayowakilisha siku zijazo. Wanapaswa kuchora ndani ya kipengele chochote watakachochagua katika hatua ya 4. Mduara mkubwa unawakilisha maono ya kutia moyo.

HATUA YA
6

Kisha, chora duara kubwa la pili kwenye kona ya chini kushoto ya chati ili kuwakilisha hali iliyopo. Chora mistari miwili iliyonyooka ili kuunganisha miduara yote miwili. Hii inawakilisha barabara kutoka sasa (chini) hadi siku zijazo (juu). Katika mduara wa chini, washiriki wanapaswa kuchora vipengele vya hali yao ya sasa.


HATUA YA
7

Katika upande wowote nje ya barabara, uliza washiriki wachore:

- angalau fursa 10 juu na
- angalau vikwazo 10 chini

HATUA YA
8

Kisha, uliza washiriki kufafanua hatua ndogo za kufikia maono. Je, wanaweza kufika umbali gani kuelekea maono ndani ya miezi 6? Njiani, waulize kuongeza hatua zinazohitajika ili kusonga kutoka hatua moja hadi nyingine na ni nani ndani ya familia yao atawajibika kwa haya, kurekebisha hatua muhimu na malengo ikiwa ni lazima.



SHUGHULI YA 6 Mti wa Usawazisho wa Jinsia

Imetoholewa kutoka kwa Reemer na Makanza (2015)

40
dakika

1-2



Lengo: Shughuli ya Mti wa Usawazisho wa Jinsia Jinsia unalenga kufafanua usawa wa kijinsia katika mchango wa kazi, na udhibiti wa mapato na matumizi katika ngazi ya kaya huku ikiepuka kutegemea dhana potofu za kijinsia. Washiriki watahusisha fursa na vikwazo katika Safari yao ya Maono na ukosefu wa usawa uliobainishwa katika mti wa usawa wa kijinsia.



Kwa nini ni muhimu? Shughuli hii huwasaidia washiriki kuelewa majukumu mbalimbali ya wanawake na wanaume ndani ya kaya. Washiriki wanaamua kama mti wa kaya uko sawia na kutambua maeneo ya kipaumbele ya kuboresha mti wa usawa wa kijinsia ili kufikia malengo yao ya urejeshaji.



Tia akilini: Shughuli hii inapaswa kuchukua takriban dakika 40. Zoezi hili lifanyike kibinafsi au na wanandoa kwa mwongozo kutoka kwa mwezeshaji. Mwezeshaji apitie polepole maelekezo hatua kwa hatua na awaaliike watu watoe mifano kwenye chati mgeuzo iliyo mbele huku watu wakichora kwenye madaftari binafsi.

Ingawa shughuli hii inaweza kufanywa kama shughuli huru, inafanya kazi vizuri kama shughuli ya ufuatiliaji wa Shughuli ya 5 - Safari ya Maono. Ikiwa unaunganisha shughuli hizi mbili, washiriki watahitaji Safari yao ya Maono kutoka kwa Shughuli 5 (uk.11).



HATUA YA

1

Tambulisha wazo kwamba kaya ni kama miti - Kaya ni kama miti - zinahitaji kusawazishwa ipasavyo ili kuzaa matunda mazuri. Ikiwa mizizi haina nguvu sawa kwa pande zote mbili, basi mti utaanguka kwenye dhoruba ya kwanza. Mti unahitaji shina thabiti na thabiti ili kushikilia matawi na matunda yake. Ikiwa matunda katika upande mmoja ni mazito kuliko upande mwingine, basi mti utaanguka na hakutakuwa na mavuno mwaka ujao.

Kukosekana kwa usawa kati ya wanawake na wanaume katika kaya ni sababu kuu ya kukosekana kwa usawa na kutofaulu katika kaya ambayo inawaacha katika hatari na kukabiliwa na kushindwa. Mara nyingi wanawake na wanaume hawashiriki kazi kwa usawa, na hivyo kusababisha mgao usiofaa wa kazi kwa kaya. Wanawake na wanaume wanaweza pia wasinufaike sawa kwa matunda, na matumizi yasiyo na faida yanaweza kusababisha 'mti' kuanguka.

Mti wa usawazisho wa jinsia unalenga kushughulikia usawa huu ili kila mtu achange na kufaidika sawa. Kisha mti wa kaya unaweza kukua imara na wenye afya na mizizi imara na matunda makubwa endelevu.

SHUGHULI YA 6 kuendelea

HATUA YA

2

Nani yuko katika kaya? (Shina)

Elezea washiriki kwamba watachora mti wenye mizizi na matawi na wanapaswa kutumia kipande kikubwa cha karatasi kwa zoezi hili. Mchoro huanza na shina. Chora mistari miwili katikati ya karatasi kwa ajili ya shina, kisha weka alama kwa kila mwanakaya mzima upande wowote ndani ya shina. Wanawake wanaofanya kazi upande wa kushoto wa shina, wanaume wanaofanya kazi upande wa kulia, na wengine katikati.


HATUA YA

3

Nani anachangia kazi gani? (Mizizi)

Chora mistari sita ili kufafanua mizizi. Mizizi miwili kwa wanawake na mizizi miwili kwa wanaume kwenye pande husika za shina. Mizizi wa kati ni kwa shughuli za pamoja.

- Katika mzizi wa nje kila upande, chora shughuli ambazo watu wa jinsia hiyo hufanya pekee yao. Kwa mfano, nini ambacho wanawake pekee yao hufanya kwa mapato, na nini ambacho wanaume pekee yao hufanya kwa mapato.
- Katika mizizi ya ndani, weka shughuli ambazo watu wa jinsia hiyo hufanya pekee yao kwa kaya, yaani, kazi za nyumbani.
- Katika mzizi wa kati, weka shughuli ambazo wanawake na wanaume hufanya kwa pamoja.
- Ukiangalia katika mizizi yote, uliza washiriki kutia mviringo shughuli zinazochukua muda mwingi na kitu ambacho wanaweza kutaka kubadilisha katika rangi ya samawati; na kutia mviringo zinazoleta mapato zaidi na kitu ambacho labda wanataka kukiweka katika rangi nyingine.



HATUA YA

4

Nani anapata matunda gani? (Matawi)

Chora mistari sita ili kubainisha matawi manne yanayolingana na kila mzizi, wanawake, wanaume na shina kuu kwa ajili ya matumizi ya pamoja ya kaya.

- Katika tawi la nje kila upande, chora alama za matumizi ya kibinafsi ambazo kila jinsi hujitengenezea pekee yake.
- Katika matawi ya ndani, weka matumizi ambayo watu wa jinsi hiyo huchangia pekee yao kwa ajili ya familia na kaya.
- Katika tawi la kati, weka matumizi hayo ambayo wanawake na wanaume huchangia.
- Ukiangalia katika matawi yote, uliza washiriki kuweka gharama kubwa zaidi katika samawati kama kitu ambacho wanaweza kutaka kubadilisha au kupunguza; na kutia mviringo yale ambao wangependa kuweka sawa katika rangi nyeusi.

HATUA YA

5

Ni nini kinachosukuma mti? (Mali na maamuzi)

Kwa upande wao wa shina, uliza washiriki kuweka alama za:

- Mali ambayo wanawake na wanaume wanamiliki - Nani anamiliki ardhi? Nani anamiliki mifugo? Nani anamiliki nyumba?
- Aina za maamuzi ambayo wanawake na wanaume hufanya - maamuzi gani hufanywa na wanawake pekee, ambayo na wanaume pekee, ambayo hufanywa kwa pamoja? Au je, mtu mmoja ndiye hutoa maamuzi kwa ujumla, au wao huketi pamoja kila mara?

SHUGHULI YA 6 kuendelezwa

HATUA YA
6

- **Mwezeshaji awaulize washiriki kama mti wao umesawazishwa.** Unaweza kutumia baadhi ya maswali yafuatayo:
 - Nani anafanya kazi nyingi?
 - Nani anamiliki sehemu kubwa ya mali?
 - Nani anamiliki sehemu kubwa ya mapato?
 - Nani hufanya maamuzi mengi?
 - Ni nani anayeshughulikia gharama nyingi

HATUA YA
7

- **Uliza washiriki kurejea kwenye Safari yao ya Maono na kujaribu kubainisha vikwazo na fursa zilizoonyeshwa kwenye mti wa mizani.** Uliza washiriki kutia mviringo wa kijani kibichi vitu wanavyovipenda kwenye mti na ambavyo vinaweza kusaidia kufikia maono. Kwa mfano:
 - Kazi zinazopaswa kufanywa kwa pamoja
 - Matumizi yanayoweza kupunguzwa
 - Mali ambayo inapaswa kugawanywa
 - Shughuli za mapato ambazo zinaweza kuongezwa au wakati unaotumika kwao kupungua.

HATUA YA
8

Uliza washiriki kubadilishana na kikundi kikubwa zaidi baadhi ya mabadiliko ambayo wangependa kufanya. Himiza washiriki kufikiria jinsi wanavyoweza kuboresha usawa katika mti wa usawa wa kijinsia na mabadiliko gani wanahitaji kufanya ili kufikia kaya iliyo sawa na endelevu.



Photo: ICRAF/Ann Wavinya



Photo: ICRAF/Ann Wavinya

KUFUNGA KIKAO

Zaidi ya warsha

Imetoholewa kutoka Leder na wengine (2016)

15
dakika

Lengo: Kufunga mazungumzo ya jamii na kueneza maarifa yaliyopatikana kwa jamii pana.



Kwa nini ni muhimu? Shughuli hii ya kuhitimisha inawapa washiriki fursa ya kutafakari juu ya yale wamejifunza na kujadili jinsi wanavyoweza kutumia maarifa hayo katika maisha yao ya kila siku. Wanaweza pia kupanga kama kikundi jinsi ya kuendelea kujadili jinsia baada ya warsha.

HATUA YA
1

Elezea washiriki kwamba warsha ni hatua ya kwanza tu, na haikusudiwi kutatua matatizo yote kwa siku moja. Sisitiza kwamba wawezeshaji hawana majibu yote, na sasa ni juu ya washiriki kueneza yale waliojifunza na marafiki na familia zao na kuendelea mazungumzo.

HATUA YA
2

Omba mmoja kujitolea kunakili maelezo huku washiriki wakibadilishana mawazo.

HATUA YA
3

Kisha, uliza washiriki kueleza jinsi watakvotumia yale waliojifunza kwenye warsha. Wanaweza pia kuchagua kubadilishana baadhi ya mambo katika Mti wa Usawazisho wa Jinsia ambayo wanataka kubadilisha kutoka kwa zoezi la awali na jinsi wanavyopanga kuyatekeleza. Himiza washiriki kuepuka kurudia majibu.

Maswali ya ziada ya kuhimiza majadiliano:

- Ni shughuli gani au mjadala gani ulikufanya ufikirie zaidi? Kwa nini?
- Ungewaambia nini marafiki au jamaa zako kuhusu tulichojadili kwenye warsha? Unafikiri wangeitikiaje?
- Unafikiri kwamba mahusiano kati ya wanaume na wanawake yatabadilika katika siku zijazo? Je, mabadiliko hayo yataonekana, na unafikiri yatasababishwa na nini?

HATUA YA
4

Funga warsha kwa kumshukuru kila mtu kwa muda na nguvu zao na kueleza matumaini kuwa siku hiyo imekuwa ya kusisimua na yenye mafanikio kwao. Wakumbushe kwamba huu ni mchakato unaoendelea na kwamba wanaweza kuendelea kufanya kazi ili kufikia malengo yao zaidi ya mafunzo.

Viungo na Rasilimali Muhimu

1 Somo la mtandaoni kuhusu Jinsia na ushirikishaji katika urejeshaji mandhari ya msitu (Mpango wa Utafiti wa CGIAR kuhusu Misitu, Miti na Kilimo misitu)

- Somo hili, liliandaliwa na wataalamu wa jinsia, linakusanya utafiti, tafiti za kifani na mapendekezo ya vitendo kutoka kwa taasisi zinazohusika na urejeshaji wa mandhari ya misitu.
- Madhumuni ya somo hili ni kutoa muhtasari wa kina wa ushirikishi wa kijinsia na kijamii na kujenga uwezo wa wadau mbalimbali wanaojishughulisha na kazi ya urejeshaji wa mandhari ya misitu.

2 IUCN (2017). Miongozo ya urejeshaji inayozingatia jinsia: Uangalizi wa karibu wa jinsia katika Mbinu ya Kutathmini Fursa za Urejeshaji. Gland, Uswizi: IUCN

3 Crossland, M., Paez Valencia, AM, Adeyiga, G., Chesterman, S., Magaju, C., Maithya, S., Mbuvi, C., Muendo, S., Musyoki, M., Muthuri, C., Muthuri, S., Mutua, F., Winowiecki, L. (2022) Mbinu za kuleta mabadiliko ya Kijinsia kwa Urejeshaji wa Ardhi : Masomo kutokana kwa Mchakato wa Usanifu wa Washikadau Mbalimbali katika Kaunti ya Makueni, Kenya. Nairobi, Kilimo Mseto Duniani

- Kama sehemu ya mradi uliofadhiwa na UK PACT, msururo wa warsha za washikadau mbalimbali zilifanyika ili kubuni kwa pamoja na kuongeza chaguo zinazofaa na zinazozingatia jinsia kwa ajili ya urejeshaji ardhi katika Kaunti ya Makueni, Kenya.
- Mwongozo huu unaangazia mbinu ya kuleta mabadiliko ya kijinsia iliyochukuliwa na mradi wa UK PACT, ukitoa mukhtasari wa mchakato, mapendekezo ya kuongeza mbinu hii, na mafunzo tuliyojifunza kutoka kwa warsha na matukio ya mafunzo.
- Inalenga watendaji wa urejeshaji na mipango iliyowekezwa mbinu ya kuleta mabadiliko ya kijinsia, kusaidia katika kuimarisha maarifa na ujuzi juu ya mbinu za mabadiliko ya kijinsia katika urejeshaji ardhi.

4 Video ya mradi kuhusu mbinu ya kubadilisha jinsia iliyochukuliwa na mradi

5 Mwongozo huu pia unapatikana kwa Kiingereza

Marejeleo

Mwongozo huu na shughuli zake zimetolewa na kutoholewa kutoka kwa zana kadhaa zikiwemo:

- Jost C, Ferdous N, Spicer TD. 2014. Gender and inclusion toolbox: participatory research in climate change and agriculture. Copenhagen, Denmark: CGIAR Research Program on Climate Change, Agriculture and Food Security; Atlanta GA, USA: CARE International; Nairobi, Kenya: World Agroforestry Centre (ICRAF).
- Leder S, Das D, Reckers A, Karki E. 2016. Participatory gender training for community groups: a manual for critical discussions on gender norms, roles and relations. Colombo, Sri Lanka: International Water Management Institute; Rome, Italy: CGIAR Research Program on Water, Land and Ecosystems.
- Reemer T, Makanza M. 2015. Gender action learning system: practical guide for transforming gender and unequal power relations in value chains. The Hague, Netherlands: Oxfam Novib.
- Hillenbrand E, Karim N, Mohanraj P and Wu D. 2015. Measuring gender transformative change: A review of literature and promising practices. CARE USA. Working Paper.
- Carden F, Smutylo T and Earl S. 2001. Outcome mapping: Building learning and reflection into development programs. International Development Research Centre.

Kiambatisho 1

Nafasi ya Jinsia

Imetoholewa kutoka Leder na wengine (2016)



Tia akilini: Ingawa tumetumia upandaji miti kama mfano, shughuli hii inaweza kubadilishwa kwa mazoea tofauti ya kurejesha ardhi, na sio upandaji miti pekee. Fikiria juu ya kazi tofauti za kazi na maamuzi yanayohusiana na mazoezi fulani ya urejeshaji na kuchukua na kuchapisha picha za kila shughuli. Mbadala, kama huna uwezo wa kufikia kamera/kichapishaji, unaweza kuchora shughuli kwenye kadi.

Orodha ya shughuli zinazowezezana na maamuzi ya kupata picha za upandaji miti:

SHUGHULI ZA UPANDAJI MITI	MAAMUZI YA UPANDAJI MITI	SHUGHULI ZA KILIMO	SHUGHULI ZA KINYUMBANI
Uenezaji/vitalu	Ni aina gani ya kupanda	Kulima kwa ng'ombe	Kufua nguo
Kukata miti	Mahali pa kupanda miti	Kupalilia	Ulezi wa watoto
Kupogoa miti		Kuvuna mazao	Kufagia kiwanja cha nyumbani
Kuvuna matunda	Jinsi ya kutumia mapato kutokana na kuuza bidhaa za miti	Kuchunga mifugo	Kupika
Kuhudhuria mafunzo ya upandaji miti		Kuchunga kuku	Kupata mapato nje ya shamba au kuendesha duka ndogo/biashara
Kuuza mazao ya miti	Kama kutumia bidhaa kutoka kwa miti kwa matumizi ya kinyumbani au kwa ajili ya kuuza	Kunyunyizia mimea kwa viuagugu/viuadudu	Kuuza mazao sokoni
Kumwagilia maji miche ya miti			Kuuza mifugo

Kiambatisho 2

Kujadili maigizo

Imetoholewa kutoka Leder na wengine (2016)



Tia akilini: Kadi hizi za hali na maigizo dhima yanaweza kubadilishwa kwa miktadha tofauti ya eneo na kitamaduni.

STORY

WAHUSIKA

Kupanda miche

Anne na binti zake wawili Jane na Maria walihudhuria mafunzo ya upandaji miti na kupokea miche 10 ya miti. Wanaenda nyumbani na kutaka kupanda miti hii kwa shamba la nyumbani, lakini baba yao, Samweli anakataa kwa sababu itaingilia kilimo chake. Mtoto wa Anne, James anamuunga mkono Samweli kwa sababu anaamini miti hiyo itasababisha mzozo kuhusu matumizi ya mavuno yatakapoanza kuzaa, kwa kuwa Anne ndiye anayeipanda. Tayarisha igizo la dakika 3-4 kuhusu jinsi Anne na binti yake watamshawishi mumewe na mwanawe kupanda miche aliyopokea.

Anne (mke)
Jane (binti)
Mariau (binti)
Samweli (mume)
James (mwana)

Kugawana majukumu

Katika familia ya Wambua Musa, Musa na mkewe Ruth wanashiriki kwa pamoja katika majukumu ya nyumbani kama vile kupika, kulima, kuchota maji na kutunza watoto. Wote wawili wanastarehe katika hali zao, lakini Musa anadhihakiwa na kaka zake Yohana, Daniel na Daudi kwa kumsaidia mkewe Ruth kusimamia nyumba. Kazi: Tayarisha igizo la dakika 3-4 kuhusu jinsi Musa na Ruth wanaweza kubadilisha mtazamo wa familia yake.

Musa (mume)
Ruth (mke)
Yohana (kaka)
Daniel (kaka)
Daudi (kaka)

Kukusanya rasilimali

Esther amewekeza muda na rasilimali zake katika urejeshaji wa rutuba ya udongo wa mashamba aliyotengewa. Mumewe Esther, Victor, anaona jinsi viwanja vyake vimekuwa na rutuba na tija bora na kuamua kwamba anataka kudai viwanja hivyo kwa ajili ya shughuli zake mwenyewe kwa sababu ardhi ina rutuba tena. Esther anawatafuta mama mkwe wake Lucy na shemeji yake Joyce kusaiaid kumshawishi Victor kwamba badala yake wanapaswa kusimamia viwanja vyote kwa pamoja kama familia na kuunganisha rasilimali na juhudi zao. Andaa igizo la dakika 3-4 kuhusu jinsi suala litakavyotatuliwa kati ya Esther, Victor, Lucy na Joyce.

Esther (mke)
Victor (mume)
Lucy (mama mkwe)
Joyce (dada-mkwe)

Kuchangia kwa usawa

Bustani ya mboga ya Faith, mke wa Petero inapata mapato zaidi kuliko mazao kutoka kwa kilimo chake. Faith hata hivyo anakataa kuchangia gharama za 'wanaume'. Kwa mfano, karo za shule na kununua pembejeo za shamba la familia, kwa sababu anaamini 'hili ni jukumu la mwanaume'. Maombi yake yote kwake yameanguka masikio yasiyosikia. Petero amemwalika mama mkwe wake Rose na shemeji yake Kelvin kusaiaid kumshawishi Faith kuchangia gharama muhimu za nyumbani. Tayarisha igizo la dakika 3-4 kuhusu jinsi Petero na mama mkwe wake Rose watamshawishi Faith kuchangia gharama za nyumbani.

Rose (mama mkwe)
Petero (mume)
Faith (mke)
Kelvin (shemeji)

Umiliki wa ardhi wa pamoja

Kuna mradi mpya wa urejeshaji unaoalika watu kushiriki lakini lazima waonyeshe umiliki wa ardhi kama sharti. Martha angependa kujiunga na mradi huo lakini hawezi kufanya hivyo kwa sababu shamba hilo liko kwa jina la mumewe pekee (Yosefu). Martha angependa kumwomba Yosefu majina yao wawili yaongezwe kwenye hati ya umiliki, lakini ana wasiwasi kwamba jambo hilo litasababisha ugomvi. Martha anamwomba mwanawe na binti yake (Daudi na Janet) kusaiaid kujadili mada na Joseph. Andaa igizo la dakika 3-4 kuhusu jinsi Martha, Janet na Daudi watakvyojadili mada hii na Joseph ili kuepusha migogoro zaidi na kutoa hoja ya umiliki wa pamoja.

Martha (mke wa kwanza)
Yosefu (mume)
Janet (binti)
Daudi (mwana)

